

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

Telegram "AFYA", **DODOMA**  
Namba ya Simu: +255 26 2323267  
Nukushi No: +255 22 2138060  
Barua zote zitumwe kwa **Katibu**  
**Mkuu**



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S.L.P 743  
**40478, DODOMA**

**TAARIFA KWA UMMA**

**SHINDANO LA KUANDAA JINA NA NEMBO YA MPANGO JUMUISHI WA  
UKIMWI, HOMA YA INI NA MAGONJWA YA ZINAA**

Dodoma; Novemba 10, 2023.

Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendeleza Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (National Aids Control Programme – NACP) ulioanzishwa rasmi mwaka 1988. Lengo kuu la Mpango huu ni kusimamia, kutoa miongozo na kuratibu udhibiti wa UKIMWI nchini Tanzania.

Wizara imepanga kujumuisha afua za udhibiti wa magonjwa ya Homa ya Ini na Magonjwa ya Zinaa kwenye Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI ili kuongeza tija na ufanisi katika kutokomeza magonjwa haya matatu ambayo yana muingiliano mkubwa katika njia za maambukizi.

Maboresho haya yatahitaji kubadili Jina na Nembo "**Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI**" kwenda Jina na Nembo la Mpango mpya ambao utaakisi Huduma za Udhibiti wa Ugonjwa wa UKIMWI, Magonjwa ya Homa ya Ini na Magonjwa ya Zinaa.

Ili kufanikisha lengo hili, Wizara inawakaribisha wataalam wa ubunifu, kutunga Jina jipya la Mpango pamoja na Nembo mahususi itakayoakisi shughuli za Mpango kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

1. Jina na Nembo viwe vinavyoeleweka kirahisi na vya kipekee,
2. Kifupi cha jina la Mpango kiwe rahisi kutamkwa,

3. Jina na Nembo vizingatie maadili ya Kitanzania na kuakisi shughuli za Mpango,
4. Nembo iwe inayoweza kutumika katika nyenzo za mawasiliano mbalimbali za Mpango mfano: majengo, magari, nyenzo za mawasiliano na uhamasishaji kama vipeperushi, mabango, Tovuti na mitandao ya kijamii,
5. Nembo isiwe na uhusiano na kazi yeyote ambayo imeshafanyika.

Mtu yeyote ambaye ni Raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 anaweza kushiriki katika shindano hili.

Mshiriki atatakiwa kutuma na kutoa maelezo kwa ufupi mapendekezo ya jina la Mpango jumuishi kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza pamoja na Kifupi chake. Sambamba na Nembo yenye kuakisi jina hilo.

Zawadi nono zitatolewa kwa Washindi watatu ambao nembo zao zitaakisi Mpango mpya utakaoanzishwa. Mshindi wa kwanza atazawadiwa fedha taslimu kiasi cha Shilingi 1,500,000/= Mshindi wa pili atazawadiwa Shilingi 1,000,000/= na Mshindi wa tatu atazawadiwa Shilingi 500,000/=

Hakimiliki zote za ubunifu wa nembo na majina mapya ya Mpango zitakuwa ni mali ya washiriki kabla na wakati wa mashindano. Mara baada ya washindi kupatikana, hakimiliki za majina na nembo za Mpango zilizochaguliwa na washindi kupewa tuzo zitakuwa chini ya Serikali kupitia Wizara ya Afya.

Kazi zitumwe kwa njia ya barua pepe [nacp@afya.go.tz](mailto:nacp@afya.go.tz) pamoja na jina la mshiriki na njia za mawasiliano. Mwisho wa kutuma kazi ni **Novemba 17, 2023**.

  
Englibert Kayombo

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**